# UPINZANI BAINA YA MUNGU NA UTAMADUNI

THOMAS GOLDING

AUTHENTICITY
BOOK HOUSE
PUBLISHING AS MINISTRY

*Upinzani Baina ya Mungu na Utamaduni*
Haki ya nakala © 2018 na Thomas Golding
Wahariri wachangiaji: Erin Ensinger, Fran Geiger Joslin, na Dianne L. Taylor
Kimetafasiriwa kwa Kiswahili na James Kalekwa

ISBN (4 x 6): 13: 978-1-943004-31-7
ISBN (eBook): 13: 978-1-943004-32-4

Authenticity Book House
Winterset, IA 50273
www.ABHBooks.com
abhinfo@abhbooks.com

Kimetolewa Kama *When God and Culture Clash* ©Authenticity Bookhouse, 2018

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutumia sehemu ya kitabu hiki au kutoa nakala kwa namna yoyote, taswira, kieletroniki, au kwa njia zinginezo, ambazo ni pamoja na kutoa nakala, kurekodi, unasaji au kutumia mfumo wowote wa utunzaji taarifa bila idhini ya kimaandishi ya mtoaji wa kitabu isipokuwa tu katika nukuu fupi zitumiwazo katika makala na upembuzi yakinifu.

Nukuu zote za maandiko, isipokuwa vinginevyo kwa kuelekeza, zimenukuliwa kutoka kwenye Biblia ya *Swahili Union Version*, hakimiliki © 1952, 1997: Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

Kwa sababu ya hali ya kubadilika badilika kwa mtandao wa internet, anwani yoyote ya tovuti au dokezo kwenye kitabu hiki vyaweza kuwa vimebadilika tangu kitabu kitolewa au haifanyi kazi tena.

Ubunifu wa Jarada na Schechner & Associates
Mpangilio wa kitabu umefanywa na Schechner & Associates

AUTHENTICITY
BOOK HOUSE

10 9 8 7 6 5 4 3 2 1
Kimetolewa na Authenticity Book House
*Kimechapwa nchini Marekani*

## Huduma ya Authenticity Book House

Authenticity Book House (ABH) hutoa **vijitabu vidogo kwa ajili ya mafunzo ya wachungaji.** Tunasambaza vitabu vyenye fundisho linalokubalika kitheolojia kwa wachungajia ambao wana mafunzo kidogo au hawana kabisa mafunzo ya kina ya Biblia. ABH hurahisisha Yaliyomo ili kufikia kiwango stahiki cha usomaji bila kupunguza uzito wa kweli muhimu zinazohitajika kwaajili ya mambo ya kiroho na uongozi.

Umbo dogo la vitabu vyetu hurahisisha usafirishaji na utoaji kwa bei nafuu. Kwakuwa vitabu hivi husafiri zaidi ya kile kituo cha kwanza kilicholengwa, tunaambatanisha ujumbe injili unaoeleweka, tukizisambaza habari njema kwa kadiri ya umbali ambao kitabu kitaenda.

Mfumo wetu wa utoaji wa vitabu ni wa ushirikiano wa kundi ambalo ni pamoja na wanatheolojia na waliothibitishwa wahariri, waandishi wabobevu na wafasiri, na washauri waelekezi juu ya tamaduni.ABH iv Kuhusu ABH inakusudia kutoa mtaala kamili kwaajili ya kuwajengea wachungaji uwezo. Tunatoa

machapisho mengine pia ili kuwezesha huduma yao kuwafikia maaminio wapya na washirika walio katika hali ya kurudi nyuma.

# Orodha ya Yaliyomo

Utangulizi

Sura ya Kwanza: Uchawi au Mungu?

Sura ya Pili: Dunia Yetu Imefikaje Hapa?
Nani Anatawala?

Sura ya Tatu: Kuwa Mwanadamu Kunamaanisha Nini?

Sura ya Nne: Tatizo Gani Lilitokea?
Mvuko Unaopanda Kutoka Ziwani
Mungu Anatakasa Dunia
Kuishi Ndani ya Utawala wa Giza

Sura ya Tano: Tiba ni Nini?
Ahadi ya Kwanza
Adamu Wawili
Kushinda Changamoto Katikati ya Dunia Iliyovunjika

Sura ya Sita: Ufalme wa Mungu Katika Udhihirisho
Vipi Kuhusu Utamaduni?

Kutoka Gizani Kwenda Nuruni
Namna ya Kuishi Nuruni
Mfano Uliopo wa Badiliko hai Kwenye Ndoa
Israeli na Sisi-Jamii Zilizogeuzwa

Hitimisho

Habari Njema Kwa Ajili Yako
Namna ya Kupokea Kipawa cha Wokovu
Mfano Uliopo wa Badiliko hai Kwenye Ndoa

Mwisho

# UTANGULIZI

Barabara ya vumbi ilielekea kwenye mazao, kisha sehemu ya uwazi, na hatimaye tunafika kwenye nyumba. Kikundi chetu kikasimama kwenye mkusanyiko wa vijumba vidogo, vingine vimejengwa kwa fito, vingine kwa nyasi. Vilikuwa si vya kawaida, lakini kusudi lake halikuwa wazi kwangu kwasababu niliviona ni vijumba vidogo kusema hayo ni makazi ya watu.

Kuku kadhaa waliparua na kudoadonoa ardhi, wakitarajia kujipatia mdudu mwenye ujazo. Kulikuwa na mbwa wawili wamelala kwa amani. Nilipoketi, bata mmoja aka-jitengeneza na kuegama vizuri mbele yangu. Baada ya muda wa dakika, walikusanyika watu kwenye vikundi vya watu waliojipanga kwenye nusu duara na kukalia mikeka.

Baadaye nilikuja kujulishwa ya kwamba tulikuwa kwenye nyumba ya mganga wa kienyeji na familia yake. Watu kadhaa kwenye mikeka walituzunguka, kimsingi, walikuwa ni wateja wake na hapo ni kama "Chumba cha kusubiria." Nilikaa kwenye duara na kuelezea habari ya Yesu mara mbili, ambaye alikuja

duniani kama mtoto, akafa msalabani kwaajili ya dhambi zetu, na kisha akafufuka kutoka kwa wafu. Kisha nikawauliza iwapo kuna mtu amabye alikuwa tayari kuokoka, wengi walifuatisha ile sala a toba niliyowaongoza, pamoja na yule mganga wa kienyeji, ninaamaini.

Zaidi a kitu ingine chochote, uzoefu huu wa kusema habari za Yesu kwenye kijiji kidogo cha kitanzania ndiyo ulipatia uelekeo wa andiko hili. Mawazo kadhaa yalinijia.

Kwa kuamini ya kwamba wote waliofuatisha sala ya toba walimaanisha, swali ni je ni kwa namna gani hii imani mpya ambayo ndugu hawa wameipokea itafinyanga mitazamo yao juu ya maisha ya kisiwa cha Kome? Au wataendelea kukaa kwenye chumba cha kusubiria mganga wa kienyeji, hali wakihitaji majibu ya matatizo yao, au watatafuta mtazamo wa Mungu juu ya dunia na majibu yake juu ya matatizo yao? Je, mganga wa kienyeji atabadili kazi yake au ataendelea kuishikilia kazi yake na kuachilia moyo wake na imani yake kwa imani mpya aliyoipokea?

Kila utamaduni hutengeneza namna yake ya kuyaelewa maisha binafsi na nafasi ya mtu duniani. Hii ndiyo huwa tunaita

mtazamo. Zoezi endelevu la kujenga mitazamo huendelea huko Kome kama ilivyo sehemu zingine Duniani. Hata mimi mtazamo wangu umejengwa wakati ninakua kwenye jimbo la Iowa huko Marekani.

Lakini ni kitu gani hasa hubadilika kwenye mitazamo Yesu pindi unapomwamini Yesu? Je, tunajua kuna uhitaji wa kulinganisha kile tunachojiunza kwenye jamii yetu dhidi kile kinachofundishwa na neneo la Mungu?

Mungu anataka kuumba jambo jipya ndani yetu sote pindi tuombapo kwa imani kwake. Anataka tuachane na mawazo yanayotokana na utu wetu wa kale na tuishi kulingana na kusudi lake juu ya dunia. Iwapo tutaomba maombi ya imani bila kutathmini mapokeo yetu ya hapo mwanzo ambao yanapingana na neno la Mungu, ni hatari sana kwasababu tutaujenga ukweli juu ya msingi wa uongo. Matokeo yake imani yetu itachanganyikiwa na dhaifu.

Mafunzo kwenye kitabu hiki yamejikita kwenye mtazamo wa Kibiblia na ni kwa namna gani tutajifunza kuacha mitazamo yetu ambayo haiendani na neno la Mungu. Tunapoifahamu kweli, tunakiona kila kitu kwa utofauti. Tunayaona maisha kama jinsi yalivyo

kwa uhalisia wake. Ungana nami kutazama mtazamo wa Kibiblia, na namna ambavyo tunaweza kumruhusu Mungu ayageuze maisha yetu, kutokea ndani kwenda nje.

# SURA YA KWANZA

## Uchawi au Mungu?

Ndani ya Biblia, kitabu cha Matendo huwasilisha taswira kadhaa za namna gani waaminio wapya waliiruhusu injili kuwageuza – au kutowageuza – mitazamo yao. Kwenye simulizi hizi kadhaa, uchawi umeonekana kuwa ni sehemu ya mapokeo kabla ya kuipokea Imani ya kweli kwa wale walioipokea injili.

Mfao wetu wa kwanza unapatikana kwenye sura ya nane tunapokutana na mchawi mmoja aitwaye Simoni. Simoni aliisikia injili na akamwamini Yesu Kristo. Lakini ni nini kilichofuatia baada ya hapo? Je, Simoni alibadilika mtazamo wake wa kichawi baada tu ya kumwamini Yesu? Je, aliiruhusu injili iugeuze mtazamo wake? Hebu na tujifunze simulizi yake.

Kuanzia mstari wa 5 tunamsoma mwinjilisti aitwaye Filipo alikwenda kwenye mji wa Samaria kuwafundisha watu habari za Yesu.

Filipo akateremka akaingia katika mji wa Samaria, akawahubiria Kristo. Na mkutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya. Kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu; na watu wengi waliopooza, na viwete, wakaponywa. Ikawa furaha kubwa katika mji ule.

Na mtu mmoja, jina lake Simoni, hapo kwanza alikuwa akifanya uchawi katika mji ule, akiwashangaza watu wa taifa la Wasamaria, akisema ya kuwa yeye ni mtu mkubwa. Wote wakamsikiliza tangu mdogo hata mkubwa, wakisema, Mtu huyu ni uweza wa Mungu, aliye Mkuu. Wakamsikiliza, kwa maana amewashangaza muda mwingi kwa uchawi wake. Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri Habari Njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.

Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo;

akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka. (Matendo 8:5-13)

Simoni, mchawi mstaafu, alijiwasilisha kwenyejamii kama mtu mkuu. Aliwashangaza watu kwa mazingaombwe yake. Pindi Filipo alipokuja kuhubiri, Simoni aliyasikiliza maneno yake na kuamini. Hata hivyo, inaonekana ya kwamba sehemu kubwa ya umakini wake ulielekezwa kwenye vitu ambavyo alimwona Filipo *anafanya*. Simoni akamkaribia Filipo kwasababu ya mshangao wake juu ya "Isahara na Maajabu" alivyoviona vikitendeka (mst. 13).

Mara zote watu wanaofanya mambo ya ajabu huvuta umakini wetu. Ninakumbuka kundi kubwa la watu waliojikusanya nyumbani kwa mganga wa kienyeji huko Tanzania. Walikusanyika hapo kwasababu ya uwezo wa yule mganga wa kienyeji na imani ya watu ya kwamba atawasaidia. Alikamata umakini wao. Timu yetu alipofundisha habari za Mwana wa Mungu, yesu, umakini wa watu hawa ukahama – na hata mganga wa kienyeji mwenyewe – alimgeukia Mungu.

Hebu tuendelee na habari a Simoni. Simoni alijisogeza karibu na Filipo. Alitazama pia pindi ambapo mitume wawili zaidi, Yohana

na Petro, walipokuja wakitokea Yerusalemu kuwaombea Wasamaria na kuweka mikono juu ya waamini wapya. Waamino wapya wakampokea Roho Mtakatifu kama Matokeo ya maombi ya mitume (Matendo 8:14-17). Simoni alijaribu kununua nguvu hii aliy-oishuhudia.

> Wakati Simoni alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, "Nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu."
>
> Lakini Petro akamwambia, "Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili ikiwezekana, usamehewe fikira hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona uko katika uchungu kama nyongo, na tena uko katika kifungo cha uovu."

> Simoni akajibu, akasema, “Niombeeni ninyi kwa Bwana, yasinifikie mambo haya mliyosema hata moja.” (Matendo 8:18-24)

Inawezekana hapo awali Simoni alijikimu kimaisha kwa kutumia uchawi. Biblia haituelezi ya kwamba nguvu zake alizipata kwa kuwafanyia watu viini macho au kutokea kwa mapepo. Tunachojua ni kwamba watu walimwita “Mtu huyu ni uweza wa Mungu, aliye Mkuu” (Matendo 8:10). Sasa Simoni anatafuta kununua nguvu anayoiona kwa Petro na Yohana. Najaribu kujiuliza kama aliona hii ni fursa ya kuongeza mbinu kwenye hazina yake ya mbinu za kichawi.

Hebu tuangalie kwa umakini jawabu la Ptero. Petro anamkemea Simoni na uelewa wake usio sahaihi juu ya kazi ya Mungu. Anamkea kwa nguvu Simoni ya kwamba nguvu za Mungu si kwaajili ya kuuza. Anamuambia auchunguze moyo wake kwasababu umejawa na nia ovu. Japokuwa Simoni alimwamini Yesu, lakini mtazamo wake ulikuwa si sahihi.

Simulizi hii huisha kwa maswali. Je, Simoni alimsikiliza Petro na kutubu? Je alielewa ya kwamba huwezi kununua nguvu za Mungu?

Je, alitambua ni kwa namna gani anamuhitaji Mungu ahasa ili amgueze ouvu uliomo ndani ya moyo wake?

Mtazamo wa Simoni ulikuwa umejikita kwenye nguvu za kichawi na namna gani anaweza akaongeza nguvu. Hapa, Simoni amepata wasaa wa kusikiliza maonyo ya Petro na kutubia uovu wake na kubadili mtazamo. Au angechagua kuendelea kufuata shauku yake ya kujipatia nguvu na kuharibu Mahusiano yake na Mungu. Biblia haituambii alichagua nini hasa.

Miaka kadhaa baadaye injili iliingia kwenye mji mwingine wa kichawi, Jiji la Efeso. Watu wengi walimwamini Yesu Kristo kama walivyofanya kule Samaria. Tofauti na Simoni, hata hivyo, watu hawa walichoma kila kitu kilichohusiana na mambo ya kichawi.

> Na wengi wa wale walioamini wakaja wakaungama, wakidhihirisha matendo yao. Na watu wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote; wakafanya hesabu ya thamani yake, wakaona ya

kwamba yapata fedha elfu hamsini. (Matendo 19:18-19)

Kuna tofauti kubwa! Mtazamo wa Waefeso uligeuka baada tu ya kumwamini Kristo. Hawakuwa na shauku tena ya kupata nguvu zaidi. Waliteketeza kila kitu cha kichawi walichokuwa nacho. Walitambua ya kwamba uchawi hauendani na hii imani mpya ndani ya Kristo.

Kwahiyo, ni kwa namna gani sasa Waefeso walitambua ya kwamba uchawi hauendani na imani mpya ndani ya Kristo? Matendo 19:8-10 inatueleza ya kwamba Mtume Paulo aliishi Efeso kwa miaka miwli kufundisha neno la Mungu. Waefeso walijifunza mtazamo mpya juu ya Mungu kutokea kwa Paulo. Walipoifahamu ile kweli, Waefeso waliacha mara moja kufanya kile ambacho hakikuendana na mapenzi ya Mungu. Kwa urahisi kabisa ni hivi, Mtume Paulo aliwafundisha neno la Mungu, kisha neno la Mungu liliwafundisha namna ya kuishi.

Ndivyo ilivyo hata kwetu. Tunajifunza neno la Mungu na maelekezo ya Mungu kwa ulimwengu, na hii hutufundisha kuishi vyema. Paulo anatuambia kwenye Warumi ya kwamba

mchakato wa kugeuzwa huanzia kwenye moyo na akili. Hii hupelekea matamanio kubadilika. Iwapo tuna shauku ya kuishi maisha yetu kwa mujibu wa njia za Mungu na bado tunaona matendo na mawazo yasiyoendana na hiki, tunaweza kuwapatia ushauri huu, kwa msaada wake.

> Wala msifuate kanuni za dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu. (Warumi 12:2)

Uchaguzi wa kutenda sawasawa na njia za Mungu, huwa hauji kwa mara moja. Mara kadhaa huwa tunapenda jadi fulani kwasababu tumekuwa zao. Ni kama vitu vya asili. Au, tunaogopa mabadiliko. Lakini kuishi sawa na mapenzi ya Mungutunapaswa kumwamini na kumruhusu kuigeuza mioyo na mawazo yetu.

Katika simulizi ambazo tumezisoma, uchawi umekuwa sehemu kubwa ya maisha ya watu walioisikia injili na kumwamini Yesu Kristo. Kwanini? Msomi mmoja wa Biblia, Edwin M. Yamauchi anaandika, " Kwenye dini mtu

huiomba miungu; kwenye uchawi mtu huiagiza miungu."[1]

Kwanini tunauona uchawi ni jambo la kuvutia? Mganaga wa kienyeji huwasaidia wateja wake na kuwawezesha kuwa na nguvu dhidi ya mambo yasiyo na uhakika kwenye maisha kwa kutumia matambiko na njia nyingine za kichawi. Ni kweli tunaishi maisha ambayo hatuna mamlaka ya kuyatawala mambo yajayo. Ingekuwaje kama tungekuwa tunafahamu juu ya mambo yajayo? Tungeenenda kwa hekima zaidi? Ingekuwaje kama tungeweza kuzuia nyakati ngumu tunazokumbana nazo? Je, tungeweza kujiepusha na hasara na kuongeza kutenda mambo mema? Ni kweli tunahitaji kiasi fulani cha mamlaka juu ya mambo yajayo, lakini kwani Mungu anasema nini kuhusu aina hii ya mawazo na matendo?

> Asionekane kwako mtu ampitishaye mwanawe au binti yake kati ya moto, wala asionekane mtu atazamaye bao, wala mtu atazamaye nyakati mbaya, wala mwenye kubashiri, wala msihiri, wala mtu alogaye kwa kupiga mafundo, wala mtu apandishaye pepo, wala mchawi, wala

> mtu awaombaye wafu. Kwa maana mtu atendaye hayo ni chukizo kwa BWANA; kisha ni kwa sababu ya hayo BWANA, Mungu wako, anawafukuza mbele yako. Uwe mkamilifu kwa BWANA, Mungu wako. Maana mataifa haya utakaowamiliki huwasikiliza wanaoshika nyakati mbaya na kutazama bao; bali wewe, BWANA, Mungu wako, hakukupa ruhusa kutenda hayo.
>
> BWANA, Mungu wako, atakupa nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye. Kama vile ulivyotaka kwa BWANA, Mungu wako, huko Horebu, siku ya kusanyiko, ukisema, Nisisikie tena sauti ya BWANA, Mungu wangu, wala nisiuone tena moto huu mkubwa, nisije nikafa. (Kumbukumbu 18:10-15)

Katika sehemu ya kwanza ya Biblia, Pindi ambapo Mungu aliwataka watu wake Israeli wasikie ujumbe, aliutuma ujumbe kwao kwa njia ya mwanadamu wa kawaida, mjumbe aliyetumwa na Mungu huitwa nabii. Wakati huo huo jumbe za manabii zilihifadhiwa na

kuwa Agano la Kale. Jumbe zozote ambazo Mungu alitaka watu wake Israeli walisikia kutoka kwake si kwa uchawi. Uchawi haukubaliki mbele za Mungu.

Baadae kwenye kitabu cha Kumbukumbu Mungu anawaambia wana wa Israeli yya kwamba kuna mambo ambayo Mungu ameyaficha kwetu wanadamu.

> Mambo ya siri ni ya BWANA, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele, ili tuyafanye maneno yote ya sheria hii. (Kumbukumbu 29:29)

Kuna baadhi ya maarifa ambayo ni ya Mungu tu. Mara zote huwa tunataka kujua zaidi. Lakini kwasababu yoyote ile, Mungu alichagua kutotufunulia kila kitu. Hebu tazama nusu ya pili ya mstari huo. Mungu hutufunilia kiasi ambacho kitatuwezesha kuwa watiifu kwake.

Tunaweza kuamini ya kwamba maarifa zaidi yanaweza kutusaidia kujisikia salama na wenye kutawala. Lakini tunaposoma neno la Mungu, tunatambua ya kwamba tunaishi hali tukiwa na mipaka. Mwandishi wa kitabu cha Agano

la Kale cha Muhubiri anatutia moyo tukubali mipaka yetu na tujifunze kumtumainia Mungu.

> Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake; tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao; ila kwa jinsi mwanadamu asivyoweza kuivumbua kazi ya Mungu anayoifanya, tangu mwanzo hata mwisho. Mimi najua ya kwamba hakuna jema kwao kupita kufurahi, na kufanya mema maadamu wanaishi. (Muhubiri 3:11-12)

> Na kwa ajili ya hayo yote, nikatia moyo wangu katika kuyachunguza haya; ya kuwa wenye haki, na wenye hekima, pamoja na matendo yao yote, wamo mkononi mwa Mungu; iwe ni upendo au iwe ni chuki, mwanadamu hajui; mambo yote yawapita. (Muhubiri 9:1)

Kwenye vifungu hivi tunaona mambo mawili. Kwanza, kila kitu ambacho Mungu hukiruhusu kwenye maisha yetu kina sehemu, hata kama ni mambo magumu na yale yasiyoeleweka kwa urahisi kwetu. Picha ya ujumla ni kwamba “ni njema katika siku yake.” Hebu fikiri kuhusu kimbunga. Kunapokuwa

na mvua kali tunaweza kuapata changamoto ya kutembea huku na huko au kuwa na vitu vyetu katika hali ya kukaua. Lakini hatimaye ni kwamba mvua hustawisha mambo yanayotuzunguka, husababisha mimea ipate uzuri na nguvu. Mvua huleta chakula kwa mimea. Baada ya magumu ya kimbunga, huja uzuri.

Pili, Mungu ahajakusudia tujue kila kitu, hata tu ile kujua ya kwamba nyakati ngumu zitageuka kuwa uzuri. Kama tusivyojua ni muda gani kimbunga kitaisha, hatujui hasa ni wakati gani nyakati ngumu zitageuka na kuwa uzuri. Mungu hajakusudia tujue kila kitu, lakini anatazamia sana tumwamini.

**Muhtasari:**

Tunapokubali ukweli ya kwamba hatuwezi kujua kila ktu na kuweka kila kitu chini ya utawala wetu, hii ni kupingana na mtazamo wa kichawi. Watu wanaoshiriki kwenye mambo ya kichawi hutafuta kujua kila kitu na kuwa na nguvu juu ya vitu hata ambavyo Mungu hakukusudia tuvijue na tuwe na nguv juu yavyo. Tunapoishi na mambo yasiyojulikana, jambo jema hutokeza. Tunajifunza kumwamini Mungu kwa kujiachilia zaidi.

Kama Waefeso walivyofanya, tunahitaji kujifunza zaidi kuhusu Mungu ili tuweze

kutenganisha baina ya uongo na kweli ya Mungu. Waefeso waliachana na imani za uongo za kichawi. Ni lazima tujifunze kuacha imani za kichawi pia.

Sehemu zinazofuatia za kitabu hiki zitaelezea namna ya kuulewa mtazamo wa Kibiblia ili tugundue imani zetu zisizo za kweli na tuachane nazo mara moja. Kisha tutafuata njia ya Mungu, hata nyakati ngumu zinapojitokeza au tutakapojua kila kitu tunachohitaji kukijua.

## Maswali: Sura ya Kwanza

1. Tamaduni za Wasamaria na Waefeso zilitumia uchawi kuwasaidia kuyafahamu na kuyatawala maisha. Je, utamaduni wako unatumia nini ili kuzielewa nyakati ngumu na kuzitawala?

2. Ni nini unachopaswa kufanya pale unapohofu juu ya maisha yajayo?

3. Iwapo ungeishi kwene tamaduni kama za Simoni mchawi au Waefeso, unadhani ungelipokeaje swala la kujifunza neno la Mungu?

    a. Je, mwitikio wako ungekuwa kama wa Simoni wa kutaka kununua nguvu za Mungu?

b. Au, unepokea kama Waefeso, kuwa katika hali ya hofu ya Mungu na kukusudia kuyaacha mambo yanayopingana mtazamo wa Mungu?

# SURA YA PILI

## Dunia Yetu Imefikaje Hapa?

Kwenye sura ya kwanza tumeona ni kwa jinsi gani Waefeso walijifunza kufanya mazingaombwe na kwa namna gani havikuendana na uhalisia wa kweli ya Mungu. Kama vile Waefeso walivyojifunza kutoka kwa Paulo, nasi twajifunza kweli ya neno la Mungu. Hii hutusaidia kuuelewa mtazamo wa Kibiblia. Kisha tunaweza kujitathmini mitazamo yetu na nini kinapaswa kubadilishwa.

Nimegawanya sehemu zinazofuata za kitabu hiki kwenye sehemu nne, kila sehemu inauliza na kujibu swali ili kutuwezesha kutambua namna mtazamo wa Kibiblia ulivyo.[2] Hebu tuanze.

### Dunia Yetu Imefikaje Hapa?

Tuamkapo asubuhi na kuona miti, kuku, anga, watoto, na hata sisi wenyewe, tunaona taswira ya uumbaji mkamilifu wa Mungu. Lakini ilikuwaje mambo haya yakafikia hivi?

Biblia inaanza kwa kujibu swali hilo kwenye sehemu za awali za mstari wa kwanza: “Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi” (Mwanzo 1:1). Mungu, Muumbaji ambaye hakuumbwa hakuwa na mwanzo, na hatakuwa na mwisho, ndiye aliyeumba dunia yote. Tofauti na Mungu, dunia ilikuwa na mwanzo.

Maandiko yanaelezea a kwamba Mungu Baba, Mungu Mwana (Yesu), na Mungu Roho Mtakatifu walitendakazi pamoja ili kuumba dunia yetu. Mstari unaofuata huzungumzia ni kwa namna gani Yesu alishiriki kwenye uumbaji wavitu vyote.

> Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika. (Yohana 1:1-3)

Tuna, muona pia Roho Mtakatifu alivyoshiriki kwenye uumbaji wa dunia kwenye Mwanzo 1:2 ambapo Roho ya Mungu ikatulia (kama ndege) juu ya uso wa maji.

Kama mabavyo Biblia inaanza kuelezea simulizi hii, tunagundua ya kwamba

dunia isingeweza kuwa Mahali pazuri kwa mwanadamu kuishi. Mstari wa 2 wa Mwanzo 1 huelezea matatizo mawili:

1. Dunia ilikuwa ukiwa—Ilimuhitaji Mungu ili aifinyange.
2. Dunia ilikuwa na hali ya utupu – Ilimuhitaji Mungu kuijaza.

Sehemu zinazofuatia kwenye sura ya kwanza na ya pili zinatueleza ni jinsi gani Mungu aliipatia dunia mwonekano mzuri na kwa jinsi gani alivyoijaza, yote hayo yalitendeka ili kukidhi uhitaji wa mwanadamu. Mungu aliumba dunia nzuri ya njema! Maandiko haya ya Biblia hututhubitishia juu ya nia nzuri ya Mungu kuwaelekea wanadamu. Amekusudia kutubariki.

**Nani Anatawala?**

Mungu aliumba vitu vyote na anatawala vitu vyote. Mungu hutawala juu ya vyote alivyoviumba kama mfalme.

> Nchi na vyote vilivyomo ni mali ya
> BWANA,
> Dunia na wote wakaao ndani yake.

> Maana ameiweka misingi yake juu ya
> bahari,
> Na juu ya mito ya maji aliithibitisha.
> (Zaburi 24:1-2)

> Maana kila mnyama-pori ni wangu,
> Na mifugo juu ya angani elfu.
> Nawajua ndege wote wa milima,
> Na wanyama wote wa mashamba ni
> wangu….
> Maana ulimwengu ni wangu, na vyote
> vilivyomo. (Zaburi 50:10-11, 12b)

Mamlaka timilifu ya Mungu humaanisha utawala wake kamili juu ya kila kitu. Hufanya kila linalompendeza. Hawajibiki kwa yeyote. Na hatimaye, hakuna mtu anayeweza kushinda naye ana akafanikiwa.

> Kwa maana mamlaka yake ni mamlaka ya milele, na ufalme wake hudumu toka kizazi hata kizazi; na watu wote wanaokaa duniani wamehesabiwa kuwa si kitu, naye hufanya kama atakavyo, katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye

> kuuzuia mkono wake, wala kumwuliza,
> "Unafanya nini wewe?" (Danieli 4:34b-35)

Mungu alitawala juu ya dunia (hii ni pamoja na viumbe wa kiroho na wa kimwili) hapo awali. Anatawala dunia yite hata hivi sasa. Na atatawala moja kwa moja zaidi milele ijayo.

Biblia hutusaidia kuelewa ni kwa namna gani anatawala. Upande wa kwanza, Mungu yuko tofauti na wa kipekee – mbali sana. Kanuni za asili ambazo zinaratibu maisha ya wanadamu hazimuathiri Mungu. Majanga ya asili kama dhoruba havimzuii kwa namna yoyote ile kama ilivyo kwetu. Zaburi 113:4-5 inatueleza juu ya hili:

> BWANA ni mkuu juu ya mataifa yote,
> Na utukufu wake ni juu ya mbingu.
> Ni nani aliye mfano wa BWANA,
> Mungu wetu aketiye juu…

Si kwamba aliziumba dunia kisha akaisukuma kule, mithili ya kusukuma mtumbwi majini lakini hakuna mtu ndani yake kuuongoza. Mungu, Mfalme wa uumbaji wote, huujali uumbaji wake na hutenda kazi katika hivyo. Hebu tuanze mistari ifuatayo kwa swali

lile lile kwene mistari iliyotangulia hapo juu, “Ni nani aliye mfano wa BWANA, Mungu wetu…”

> Anyenyekeaye kutazama,
> Mbinguni na duniani?
> Humwinua mnyonge kutoka mavumbini,
> Na kumpandisha maskini kutoka jaani.
> Ili amketishe pamoja na wakuu,
> Pamoja na wakuu wa watu wake.
> Humweka nyumbani mwanamke aliye
> tasa,
> Awe mama ya watoto mwenye furaha.
> (Zaburi 113:6-9)

Huu Mungu mzuri mwenye utukufu pia ni Mungu wa neema! Hapo mwanzo, aliziumba mbingu na nchi, kama vile alitengeneza mtumbwi ambao unapaswa kwenda safari. Lakini Mungu pia yumo ndani ya mtumbwi, yumo safarini pamoja nasi, akitoa mwongoz kamili wa uelekeo wa safari yetu. Biblia inatupatia taswira ya Mungu anavyowajali viumbe wake. Maandiko mengi humtaja Mungu kama mchungaji anayewajali kondoo wake. Kwenye andiko moja tunajifunza ya

kwamba kumbe Mungu huongoza na kuzitunza nyota.

> Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi; aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza wake, na kwa kuwa yeye ni hodari kwa nguvu zake; hapana moja isiyokuwapo mahali pake. (Isaya 40:26)

Jinsi Isaya anavyomuwasilisha Mungu ya kwamba hjali nyyota za angani, hii ni kuonyesha ya kwamba kutujali sisi si tatizo. Kama kwa hakika anaweza kuongoza nyota za angani ni hakika ya kwamba aweza kututunza, au kutuchunga pia. Tunaweza kumwamini Mungu ya kwamba atatutunza.

> Atalilisha kundi lake kama mchungaji, Atawakusanya wana-kondoo mikononi mwake; Na kuwachukua kifuani mwake. (Isaya 40:11)

**Muhtasari:**

Kwahiyo, ni kwa namna gani dunia yetu ilifikia hapa na ni nani ayaitawala dunia? Msingi mmoja wa mtazamo wa Kibiblia ni

uhalisia ya kwamba wanadamu wanaishi katika dunia nzuri iliyoandaliwa na muumbaji mwema. Mungu, mfalme wetu, huitunza dunia aliyoiumba na huwatunza kwa upendo wale wote waishio ndani ake.

## Maswali: Sura ya Pili

1. Tafakari kuhusu ukuuu wa Mungu. Aliumba dunia yote pasipokuwa na malighafi, kwa kutumia maneno tu. Huyu Mungu asiye na mwanzo wala hatakuwa na mwisho. Je, unajisikia salama kwenye uangalizi wake?

2. Hebu kumbuka ule mfano wa mtumbwi kisha fikiri. Hebu elezea nyakati ambazo uiusikia uwepo wa Mungu kwenye "mtumbwi" wako.

3. Elezea nayakati ambazo ulijsikia ya kwamba umebaki peke yako kwenye mtumbwi. (Hata nyakati za sasa, Biblia inatuhakikishia ya kwamba Mungu anabaki kuwepo pamoja nasi.)

# SURA YA TATU

## Kuwa Mwanadamu Kunamaanisha Nini?

Sasa tutaangalia n nini hasa maana ya kuishi kama mwanadamu kwenye dunia ambao Mungu aliziumba. Kwa mara nyingine tena kitabu cha Mwanzo kinatusaidia.

Mungu anatupa taarifa muhimu kuhusiana na sisi wenyewe kwenye Mwanzo 1. Anatuambia ya kwamba alituumba kwa mfano wa sura yake. Hakuna sehemu yoyote yauumbaji wake ambayo imevaa sura yake, ni mwanadamu tu.

> Mungu akasema, Na tumfanye mtu mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wabaharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutamabaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. (Mwanzo 1:26-27)

Kwa mujibu wa mstari wa 26, Mungu aonyesha utofauti baina ya wanadamu na wanyama na wanadamu. Japokuwa kuna nyakati tunaona mambo yanayofanana kama vile pumzi, kutembea, na kuzaliana, lakini Mungu anatuambia ya kwamba wanadamu I wa tofauti. Wanadamu hubeba sura ya Mungu. Wanayama hawana. Kubeba sura ya Mungu hakutufanyi tuwe Mungu, hatahivyo kama vile ambavyo wanyama wana mambo kadhaa yanayofanana nasi na kuna tofauti baina yao na sisi, ndivyo nasi wanadamu kuna namna tunafanana na Mungu na kuna maeneo ambayo tuko tofauti naye.

Mungu anafanyya kitu kingine kizuri na wanadamu. Katika siku ya sita ya uumbaji Mungu aliwabarikia wanadamu na kuwapa maagizo matano.

> Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, Mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. (Mwanzo 1:28)

Hii maana yake ni nini? Mungu, Mfalme wa uumbaji wote, umeukabidhi utawala wake juu ya dunia kwa kiumbe wake, mwanadamu. Wanadamu wanabeba jukumu la kumwakilisha Mungu na kuitunza dunia. Mungu aliwapatia Adamu na mke we majukumu yafuatayo wayatekeleze:

1. Zaeni (fanyeni kazi za maana, za uzalishaji duniani).
2. Mkaongezeke (kuwa na familia).
3. Mkaijaze nchi (muifurahie hii dunia na msambae na kuenea Duniani kote).
4. Mkaitiishe dunia (kuhakikisha kuna utaratibu na utulivu kwa uumbaji wa Mungu).
5. Mkatawale nchi (kumwakilisha mfalme wenu—Mungu).

Mwandishi wa Zaburi 8 anaelezea mshangao wake juu a uumbaji na majukumu ambayo Mungu anawapatia wanadamu. Nashangazwa na uhusiano baina ya Mungu na mwanadamu. Labda nawe upo kwenye hali hiyo ya mshango:

> Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako,
> Mwezi na nyota ulizoziratibisha;

Mtu ni kitu gani hata umkumbuke,
Na binadamu hata umwangalie?
Umemfanya mdogo kuliko Mungu;
Umemvika taji la utukufu na heshima;
Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako;
Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.
Kondoo, na ng'ombe wote pia;
Naam, na wanyama wa porini;
Ndege wa angani, na samaki wa baharini;
Na kila kipitacho njia za baharini. (Zaburi 8:3-8)

Tukirejea kwenye Mwanzo sura ya 2, Mungu anampatia Adamu jukumu lake la kwanza – kuwapatia majina wanyama. Jukumu hili lina uzito mkubwa. Tunapokipatia kitu au jambo jina, tunaonyesha mamlaka juu yake. Kitu gani huwa tunafanya baada tu ya watoto wetu kuzaliwa? Tunawapatia majina kisha tunawajibika kuwatunza. Kumpatia Adamu mamlaka ya kumwakilisha, Mungu anampa Adamu jukumu lake kwenye bustani ya Edeni.

> BWANA Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina

> alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake. Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; … (Mwanzo 2:19-20a)

Jambo jingine jipya linajitokeza baada ya Adamu kuwapatia majina wanyama. Adamu alikuwa na mtafuta mtu mwingine wa kufanana naye, mwingine aliyeumbwa kwa sura ya Mungu. Hakukuwa na kumbe wa namna hiyo. Biblia inatuambia a kwamba Mungu aliumba mwanamke kutokea kwenye ubavu wa Adamu kisha akamuwasilisha kwake.

Adamu alionyesha mshituko wa hali ya juu alipomuona mwanamke. Akamwelezea kama "mfupa katika mifupa yangu…" Mungu aliyatengeneza mahuasino haya baina ya mwanamume na mwanamke ili kwamba "nao watakuwa mwili mmoja" (Mwanzo 2:23-24). Kwenye Mwanzo 1 Mungu anatueleza ya kwamba mwanamume na mwanamke *wote kwa pamoja* ndiyo hukamilisha mfano wake.

> Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba,

mwanamume na mwanamke aliwaumba. (Mwanzo 1:27)

Hii inaweza kuonekana kama inachangana, lakini Mungu anatuonyesha taswira yake hapa. Sehemu ya taswira ya Mungu ni "moja" iliyojengwa na mkusanyiko wa zaidi ya moja. Mungu yupo katika hali ya utatu ndani ya mmoja (Baba, Mwana na Roho Mtakatifu). Kwa namna hiyo hiyo, "mwanadamu" hawezi kukamilika bila kuwa na mwanamume na mwanamke. Hii ndiyo sehemu muhimu: si mwanaume au mwanamke ambaye ni bora kuliko au duni zaidi ya mwenzake katika kuiwakilisha taswira ya Mungu. Kwa pamoja wanabeba sura ya Mungu, na kwa pamoja wanafanya kazi kuitawala dunia. Kumbuka, wanaume na wanawake wavikwa sura ya Mungu.

**Muhtasari:**

Jambo la pili la msingi katika mtazamo wa Kibiblia ni uelewa wa namna gani Mungu aliumba wanadamu ili kuishi kwenye uumbaji wake na kuwakilisha Yeye humo. Tofauti na wanyama, Mungu aliwavika wanadamu sura yake. Aliwapatia pia jukumu la kufanya:

Kuenea Duniani kote na kutunza uumbaji wake.

## Maswali: Sura ya Tatu

1. Iwapo wanaume na wanawake wanawakilisha sura ya Mungu, je wanapaswa kuhusiana vipi?

2. Je jinsia moja ni bora kuliko nyingine, au Mungu huwajali wote kwa usawa?

3. Unashiriki vipi kwenye jukumu ambalo Mungu alimpatia Adamu?

4. Ni kwa namna gani unaweza kuitunza dunia na kuifanya kuwa bora?

# SURA YA NNE

## Tatizo Gani Lilitokea?

Mpaka hivi sasa, tumekwishajifunza ni kwa namna gani mtazamo wa Kibiblia huwaweka wanadamu kwenye ulimwengu mzuri ulioandaliwa na muumbaji mwema. Uumbaji wa wanadamu unawakilisha kiwango kikubwa cha uumbaji wa Mungu. Mungu aliwabarikia wanadamu na kuwaagiza mwanaume na mwanamke wote kwa pamoja kuitawala dunia yake Mungu.

Lakini kuna namna mambo yakaharibika sana! Wanadamu watawalapo huwa tunakumbana na maumivu na tunajionea namna ambavyo watu wanatawaliwa na wenzao. Makabaila mbalimbali yametawalana; nchi zimeanzisha vita; familia na jamaa zimegawanika. Na hata mazingira yetu – dunia yetu – huchafuliwa na kujawa na uchafu kila siku.

Vita, magonjwa, maumivu, na hata mauti vimeivamia dunia yetu. Punde si punde huzuni huharibu sura ya kila mtu. Dunia

njema ambayo Mungu aliziumba na mfano wa sura yake ndani ya mwanadamu hupotea na kupoteza tumaini. Kwanini?

Kwa mara ningine tena, tunakutana na amajawabu ndani ya kitabu cha Mwanzo. Mwanzo huelezea nini kilitokea kwenye mbingu na nchi pindi Adamu na Hawa walipotenda dhambi. Lakini pia kinatueleza ni nini kilitokea kwa ukoo uliopatikana kutokea kwa watoto wa Adamu na Hawa.

Pindi Adamu na Hawa walipochangua kutomuheshimu Mungu, dunia ilibadilika punde. Kutotii kulileteleza ugumu wa maisha. Wanadamu wanaendelea kupambana na ugumu wa maisha hata hivi leo. Kuzaa kukawa ni jambo lililoambatana na ugumu kwa mwanamke. Kufanya kazi kukaambatana na ugumu kwa mwanaume. Badala ya kukamilishana, hizi jinsia zikaanza kupigana vita. Tunajua baadae kwenye vizazi baada ya vizazi, mtu hufa na kuyarudia mavumbi ambayo Mungu alimuumba kwayo.

Mtume Paulo anasema, "viumbe vyote vilitiishwa chini a ubatili" (Rum. 8:20a) na viumbe vyote "vimewekwa katika utumwa wa uharibifu" (mst. 21). Dunia "inaugua pamoja na ina utungu hata sasa." (mst. 22).

Je, unayashuhudia haya kwenye mazingira yako? Je, unaona familia zilizovunjika? Je, huwa unakumbana na nyakati ambazo ardhi haina maji ya kutosha kuchipusha mazao ya chakula? Haya yote yanatuonyesha ni kwa namna gani uumbaji mzuri ulivyolaaniwa pindi dhambi ilipoingia Duniani.

**Mvuko Unaopanda Kutoka Ziwani**

Ulishawahi kuamka asubuhi moja na kuuona mvuke ukiinuka kutokea ziwani kabla jua halijachomomoza na kuupoteza kwa kuuchoma? Ulishawahi kupika chakula na kuona namna ambavyo mvuke huinuka kutoka kwenye chakula cha moto? Ukitaka kuukamata huo mvuke ili uutunze, utachanganyikiwa. Mvuke hupotea mara moja tu pindi unafunga mkono wako kuutunza mvuke.

Mwandishi wa kitabu kimoja cha Agano la Kale kiitwacho Muhubiri anatumia taswira hii ili kutusaidia kuelewa dunia yetu ilivyochanganyikiwa. Anatumia neno "upepo" au "ubatili". Kama jinsi tusivyoweza kuukamata mvuke unatokeza juu ya moto, hatuwezi kuutunza – au kuelewa kwa utimilifu – matukio katika maisha. Kwa mfano, je tunajaribu kuelewa kwa kaisi gani kifo cha mtoto mchanga

au mauaji ya kikatili ya mtu asiye na hatia? Matukio yanayoendelea yanaweza kutuacha hali tumechanganyikiwa, tumecurugwa, wenye huzuni, hasira au hata masononeko. Mfumo wa Mungu wa haki siku zote haueleweki kwetu.

> Kuna ubatili [upepo] unaofanyika juu ya nchi; kwamba wapo wenye haki nao wapatilizwa kama kwa kazi yao waovu; tena wako waovu, nao wapatilizwa kama kwa kazi yao wenye haki. Nami nikasema ya kuwa hayo nayo ni ubatili [upepo]. (Muhubiri 8:14)

Muhubiri huunganisha ubatili [upepo] na neno "kujilisha upepo." Kama jinsi ambavyo hatuwezi kuutunza mvuke kwenye viganja vyetu vya mikono, ndivyo ambavyo hatuwezi kushiba upepo. Maneno haya yanamaanisha ya kwamba kila siku za maisha yetu huwa zimeambatana na shughuli zisizo na matunda. Kujilimbikizia na mali nyingi za dunia ni sawa na kuigiza hili zoezi la "kujilisha upepo." Kwasababu mtu anayejilimbikia mali hufa na kuiacha mali hiyo kwaajili ya watu wengine.

> Nami nikaichukia kazi yangu yote niliyojishughulisha nayo nayo chini ya jua; maana sina budi kumwachia yeye atakayenifuata. Naye ni nani ajuaye kama huyo atakuwa mwenye hekima au mpumbavu? Hata hivyo atatawala juu ya kazi yangu yote niliyojishughulisha nayo, ambamo ndani yake mimi nimeonyesha hekima chini ya jua. Hayo nayo ni ubatili. (Muhubiri 2:18-19)

Tunakumbana na ukweli mchungu. Watu wote hufa. Hata watu bora sana nao hufa. Muhubiri 12:7 huelezea hivi: “Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, Nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa.”

Kwetu, maisha yameambatana na maumivu wa kifo baada a Adamu na Hawa kutenda dhambi. Na tunakumbana na ukweli mwingine mchungu. Kuna jambo lilijitokeza kwenye mbingu na nchi kwasababu ya dhambi.

> Yaliyopotoka hayawezi kunyoshwa, Wala yasiyokuwapo hayahesabiki. (Muhubiri 1:15)

> Tafakari vyema kazi yake Mungu. Kwasababu ni nani awezaye kukinyosha kitu kile alichokipotosha (kukunja) yeye? (Muhubiri 7:13)

Subiri. Andiko la mwisho limetueleza ya kwamba Mungu ndiye aliyeipotosha (kukunja) dunia? Ndiyo. Alifanya hivyo kama majibu kwa dhambi iliyotendwa na Adamu na Hawa, Mungu akaipotosha (kukunja) dunia! Dunia haienendi tena katika mfumo ule ambao ilipaswa kuenenda tangu awali.

Mwandishi wa Mhubiri anaendelea mbele na kuzngumzia hali ya mioyo yetu:

> Bila shaka hakuna mwanadamu mwenye haki hapa duniani, ambaye afanya mema, asifanye dhambi. (mst. 7:20)
>
> Mungu amemfanya mwanadamu mnyofu, lakini wamebuni mavumbuzi mengi. (mst. 7:29)

Sasa tunaweza kuona kwa urahisi nini kilitokea kwa uumbaji mzuri wa Mungu na wanadamu. Japokuwa aliumbwa akiwa

"mnyoofu," wanadamu walichagua kujipotosha (kujikunja) wenyewe na *Mungu akaipotosha (akaikunja) dunia kama majibu ya kujikunja kwao.*

**Mungu Anatakasa Dunia**

Japokuwa Mungu aliipotosha (aliikunja) dunia, bado anaipenda na anatenda kazi pamoja na viume wake. Kwene Mwanzo 6 tunajifunza ya kwamba matendo ya wanadamu yalikuwa maovu sana. Lakini Mungu akaamua "kuitakasa" dunia kwa mafuriko, na kumuokoa Nuhu na familia yake.

> Dunia ikaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa na dhuluma. Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika; mana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake mwenyewe Duniani. (Mwanzo 6:11-12)

Tunaweza kudhani ya kwamba baada ya Mungu kuitakasa dunia kwa gharika ingetatua tatizo, lakini Nuhu na familia yake walibeba ungonjwa wa dhambi na kuhamishia kwenye dunia iliyosafishwa. Kwa mara nyingine tena, dhambi ikaenea.

Baadaye, Mungu akanza kutenda kazi na "familia mpya." Akatenda kazi na familia

ya Ibrahimu na kufanya taifa kutokea kwa mtu huo – Israeli. Lakini kwa mara nyingine tena, historia ya Agano la Kale inaonyesha ya kwamba taifa la Israeli lilisambaza ugonjwa huo huo wa dhambi na kuiharibu nchi ambayo Mungu aliwapatia. Ugonjwa bado unasambaa kwa wanadamu, na dunia inabaki kuwa imepotoshwa.

**Kuishi Ndani ya Utawala wa Giza**

Tunakumbana na nini tunapoendelea kuishi kwenye dunia hii iliyopotoshwa? Kwanza, Mtume Paulo anauelezea ulimwengu baada ya dhambi kuingia "utawala wa giza" (Wakolosai 1:13; Matendo 26:18). Watu wengi hawatambui hilo, lakini wanazaliwa na kuwa raia wa ufalme unaowanyanyasa. Dunia ya giza tunayoishi ndani yake hufurahia imani na maadili maovu. Sehemu kubwa ya watu ulimwenguni hufuata imani na maadili hayo.

Waefeso 2:2-3 huzungumza kuhusu watu wanaoishi kwa kufuata "kawaida" zilizowekwa na ulimwengu. Kawaida za ulimwengu hutofautiana baina ya kizazi hadi kizazi na utamaduni mmoja na utamaduni mwingine. Lakini kuna jambo moja linafanana katika kawaida hizi: Tunamwacha Mungu na

kutomuhusisha kwenye namna yetu ya kuwaza na kutenda.

Paulo anamwelezea mtawala wa ufalme huu wa giza. Anamtaja kama "mfalme wa uwezo wa anga, roho ule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi" (Waefeso 2:2). Kwenye 2 Wakorintho 4:4 anamtambulisha kama "mungu wa dunia hii." Yesu anazungumza juu ya "mkuu wa dunia hii" kwenye kitabu cha Yohana (12:31; 14:30; 16:11). Majina yote haya yanamtaja Ibilisi, au Shetani.

Mtazamo wa Kibiblia juu ya ulimwengu unatuonyesha juu ya uhalisia wa viumbe engine wa kiroho waitwao mapepo. Mapepo hushirikiana na Shetani na humpinga Mungu. Hapo awali walikuweko kama malaika walioumbwa na Mungu. Wakati fulani, waliasi. Baadhi ya mapepo yanashikilia nafasi kubwa za kimamlaka kwenye mfumo wa utawala, kama serikali, na Shetani ndiye kiongozi mkuu.

> … kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. (Waefeso 6:12)

Si tu kwamba tunaishi katika ulimwengu wa giza, uliopotoshwa, lakini pia tunapambana na adui. Adui anatawala kama adui wa kwanza kwa mwanadamu. Biblia inatueleza ya kwamba tangu mwanzo Ibilisi, Shetani, alitumia uongo kama silaha yake ya nguvu. Aliutumia kwenye bustani ya Edeni alipowaangusha Adamu na Hawa. Historiaya wanadamu inaonyesha amekuwa akitumia uongo na hufanya hivyo hata leo. Kwenye kitabu cha Yohana, Yesu anamtaja Ibili kama "mwongo na baba wa huo ...hakuna iliyo kweli ndani yake.  Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe, kwasababu yeye ni mwongo na baba wa huo" (Yohana 8:44b).

Si tu kwamba shetani husema uongo, bali huujaza uliwemngu na uongo mwingi. Uongo huonekana ni mzuri sana, watu huchagua kuuamini. Uongo hushabikiwa na ukweli hutupwa kando. Tamaduni zote zimejengwa kweye mchanganyiko wa kweli na uongo.

Kwa mfalo, nchini Marekani watu wengi huamini ya kwamba Mungu yupo. Hta hivyo, wengi wao hawaamini ya kwamba wanapaswa kusoma Biblia ili kumfahamu Mungu kwa ukaribu zaidi. Wanapenda kutengeneza mawazo yao kuhusiana na Mungu na mapenzi

yake juu ya uumbaji wake. Huu ndiyo mchanganyiko wa kweli na uongo – Ukweli: Mungu yupo. Uongo: Watu hudhani wanaweza kumweleza kwa akili zao.

Vizazi huja na kuondoka, kila kimoja huutazama ulimwengu kwa kiwango fulani cha kweli na uongo. Ibilisi (Shetani) kwa kutumia uongo wake, anatamani kuwapotosha watu wa tamaduni zote waende mbali na Mungu, kama vile mfano ulioelezewa hapo juu. Kwa kutumia uongo wake na upinzani kwa Mungu, Shetani ndiye chanzo chasehemu kubwa ya uovu na maumivu duniani.

Umegundua ya kwamba nimesema *sehemu kubwa* ya uovu ya duniani. Nini kingine husababisha uangamivu tunaoushuhudia kila siku? Wanadamu huchangia uangamivu wa dunia hii. Miili etu, au namna yetu ya kuwaza kibinadamu imejawa na dhambi. Kwasababu hiyi, tunatenda maovu. Mtu anapotenda katika hali ya mwili, tunatenda kile ambacho huja kwa asili. Mwili hutaka kutenda kile unachotaka, kupata kile unachotaka kupata. Ubinafsi, mawazo yenye kiburi na matendo huzaliwa kutokea hapa, ambayo huchangia kwenye uangamivu wa dunia.

Matatizo mawili ambayo tumeyajadili, giza la dunia na mtawala wa dunia, hivi huishi nje yetu kama wanadamu (isipokuwa pale ambapo mtu huingiwa na mapepo na kuyamiliki maisha ya mtu husika). Mwili, kwa upande mwingine, ndiyo sehemu yetu. Kwasababu dhambi imo ndani yetu hivyo ni lazima kuishughulikia kila siku.

Shetani hupenda kutumia asili yetu ya dhambi kupigana nasi. Anatambua wazi ya kwamba tuna mapambano ndani yetu ya kumtii Mungu na kusema hapa kwa mwili. Pindi tunapochagua kumpuuza Mungu, Shetani hutusaidia kwa ukarimu na kutuaminisha kwenye uongo ya kwamba kuishi mbali na Mungu ni jambo bora zaidi.

Nini hasa ni chanzo cha uharibifu na uovu kwenye maisha?

1. Adui yetu, Ibilisi.
2. Dhambi ya Adamu na Hawa na kuenea kwa dhambi kutoka kizazi kimoja kwenda kingine na tamaduni hadi tamaduni.
3. Dunia yetu yenye giza, iliyokunjwa na Mungu kama Matokeo ya dhambi ya Adamu na Hawa.

**Muhtasari:**
Kuielewa na kusihi kwenye dunia yenye uovu tunapaswa kutambua kile tunachokumbana nacho ambacho hupingana na uumbaji asilia wa Mungu. Kwa namna ya nje tunakumbana na vikwazo viwili: Dunia iliyopotoshwa na Shetani. Tunakumbana na kikwazo kimoja ndani yetu: Hali yetu ya miili ya dhambi. Pamoja na yote, Mungu anatutaka tuishi maisha matakatifu. Lakini inawezekanaje? Tuendelee kusoma.

## Maswali: Sura ya Nne

1. Ni mambo gani mitatu ambayo tunapambana nayo sana tangu anguko la Adamu na Hawa?

2. Yapi baina ya hayo ambayo hukuletea mapambano makubwa?

3. Kwenye sura hii nilitambulisha mambo magumu ya kimaisha. Nilihitimisha na tumaini ya kwamba Mungu atatupatia tunavyohitaji ili tuishi kwenye dunia hii. Taja eneo moja la maisha yako ambalo linahitajika tumaini na kujua ya kwamba Mungu atakusaidia ulishinde giza.

# SURA YA TANO

## Tiba ni Nini?

Namna gani tunaweza kutoka kwenye njia ya kuvunjika na kukosa usalama kuingia kwenye njia ya ukamilifu na usalama? Ulimwengu wetu unaougua unaweza kupata uponyaji? Je, Mungu atakunjua kile ali-chokikunja mwenyewe kwa sababu ya kutotii kwa mwanadamu? Mungu anayajibu maswali haya kwenye Biblia pia.

**Ahadi ya Kwanza**

Shetani alionekana kwa Adam na Hawa kama nyoka alipowashinda katika bustani ya Edeni (Mwanzo 3). Kwa sababu hii, Mungu alimlaani nyoka na ardhi. Kimsingi Mungu hakuwalaani Adam na Hawa. Na katika kutowalaani Adam na Hawa, Mungu aliwapa ahadi, nguzo ya tumaini japo uumbaji ungeishi kwenye laana na maisha yangekua magumu. Mungu alipomhukumu nyoka, alisema:

> Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake. Huo utakuponda kichwa na wewe utamponda kisigino. (Mwanzo 3:15)

Hapa Mungu alikua anadokeza kuhusu wakati ujao. Huu mstari unatuelezea kwamba nyoka (anayemwakilisha shetani) ange-piganakinyume cha familia ya Adm na Hawa pamoa na uzao wao. Hatimaye, moja ya uzao wao ungeingia ulimwenguni na kupata jeraha kutoka kwa shetani. Mtu huyu huyu angekanyaga kichwa cha shetani na kumuangamiza kabisa. Hapa Mungu anawapa dokezo Adamu na Hawa kuhusu Yesu Kristo "Adamu wa pili."

**Adamu Wawili**

Agano jipya linafunua habari nzima kuhusu Adamu wa pili. Adamu wa kwanza (Adamu wa uumbaji) alileta dhambi, mateso, magomjwa na kifo ulimwenguni. Alisababisha wanadamu kupoteza makao yao katika katika bustani ya Edeni na kupoteza mamlaka yao ya utawala juu ya dunia.

Adamu wa pili anafanya kinyume. Yeye analeta msamaha, uponyaji, furaha, uzima na

mabadiliko kwa wanadamu. Adamu wa pili (Yesu) atarejesha upya mbingu na nchi pia.

Mtume Paulo anawaelezea Adamu wa kwanza na wa pili kama hivi:

> Lakini sasa Kristo amefufufkakatika wafu, limbuko lao waliolala (waliokufa). Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhakika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa katika Adamu wote wanakufa, kadhalika katika Kridto wote wanahuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake: limbuko ni Kristobadaye walio wake Kristo, atakapokuja. Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote na mamlaka yote na nguvu. Maana sharti amiliki yeye, hata aweke maadui wake wot echini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakyebatilishwa ni mauti. (1 Wakorintho 15:20-26)

Wakati mwingine huwa tunaufikiria wokovu kwa ufinyu sana. Tunafikiria kuhusu jinsi gani wokovu unaleta msamaha wa dhambi na umilele pamoja na Mungu mbinguni.

Lakini Yesu anaahidi zaidi ya hapo. Ana ahidi kurejesha upya ulimwengu wote.

Kumbuka tulivyojifunza katika kitabu cha warumi sura ya nane (Warumi 8) kwamba “viumbe vyote vimetiishwa chini ya ubatili” (mst. 20) na mpaka sasa viumbe vyote bado “viko chini ya utumwa wa uharibifu” (mst. 21)? Siku moja, mateso na kuugua kwa viumbe vyote kutaisha. Utumwa wa uharibifu utakoma. Furaha, bila huzuni itaanza. Paulo anaelezea, “kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu” (mst. 19).

## Kushinda Changamoto Katikati ya Dunia Iliyovunjika

Mpaka mateso ya viumbe yakome, tunahitaji kujifunza namna ya kuishi kwenye ulimwengu uliopindwa na wakati huo huo tukimuheshimu Mungu. Kama Paulo alivyowafundisha Waefeso namna ya kufanya hivi, Biblia pia inatufundisha. Nini mtazamo wa kibliblia kuhusu namna ya kuishi duniani, bila kujari ni wapi na lini tunaishi?

Agano jipya kwenye kitabu cha Wakolosai inatuambia Mungu Baba “alituokoa katika

nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake" (1:13).

Fikiria kwa namna hii. Fikiria unamiliki pasipoti. Pasipoti yako inaelezea mamlaka ya nchi unayotokea- inakutambulisha wewe pamoja na chi hiyo.  Kila mwanadamu ana paspoti inayomtambulisha kuwa yeye ni wa ufamle wa giza. Tulipozliwa, mimi na wewe, tulimilikiwa na ufame wa giza. Fikiria sasa Mungu anachana ile pasipoti na kukupa pasipoti mpya inayosema wewe ni wa milki ya Ufalme wake. Kama tunamwamini Yesu hatuna haja ya kufikiria hivi. Sisi sio wa ulimwengu huu wa giza tena wala sharia yake haifanyi kazi juu yetu. Sasa tunafurahia uraia wa mbinguni, ijapokua kwa muda tunaishi hapa duniani kama wageni (1 Petro 1:1; 2:11).

Kwa hiyo sisi sio wa ulimwengu huu wa giza tena. Lakini vipi kuhusu adui yetu, shetani na ulimwengu wake wa kipepo? Agano jipya linatwambia kuwa Yesu anatawala kwa mamlaka kuu na anaketi mkono wa kuume wa Mungu. Anatawala juu ya shetani, ambaye si kama Yesu, aliyepo kama kiumbe kilichoumbwa.

Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zetu. Waraka wa kwanza wa Petro sura ya tatu (1

Petro 3) anatwambia kwamba aliziendea roho zilizokua kifungoni (kama malaika waliomuasi Mungu wakati wa Nuhu) na akatngaza ushindi juu yao (mst. 19). “Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika, enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake” (mst. 22). Ndio, shetani na mapepo yake bado yana nguvu na wakati mwingine huwa tunaziona. Lakini Yesu huziwekea mipaka hizo nguvu. Yesu alimshinmda shetani na mapepo yake kwa kifo chake msalabani na ufufuko wake kutoka katika wafu.

Sisi bado tunapambana ndani yetu wenyewe na miili na dhambi zetu. Tiba ya mwili ni Roho Mtakatifu. Mungu humpa Roho Mtakatifu kila mtu anayemwamini Yesu. Roho hutsaidia kushinda mambo yanaayotukwamisha kiuasilia.

> Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa z mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili, kwa maanza hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayoyataka. (Wagalatia 5:16-17)

Mwanzoni kwenye hiki kitabu tulizungumza kuhusu muunganiko wa Mungu na uumbaji wake. Hii inabaki kuwa kweli. Mtume Paulo anasema kwenye kitabu cha Warumi 5-8 kwamba kama sasa sisi ni watoto wa Mungu basi Yeye yuko upande wetu. Alitupa zawadi bora ambayo hatukuwahi kuipokea- mwanawe wa pekee, aliyekufa kwa ajili ya dhambi zetu. Kama Mungu alimtuma mwanawe pekee basi hawezi kutuzuilia chochote tunachokihitaji ili kuishi maisha ya kumpendeza.

Mungu anatupa uwezo wa kushinda mwili kupitia Roho wake Mtakatifu. Kuenenda kwa Roho haimaanishi kuishi maisha makamilifu. Haimaanshi kujitahidi kwa bidi kushika sheria kwa nguvu zako. Tunapojaribu kuishi maisha maisha makamilifu kwa nguvu zetu tunaishia kuficha na kufunika makossa yetu. Hatuwezi kuzalisha utauwa kutokea ndani yetu sisi wenyewe. Kufanya hivyo kunapelekea kuchanganyikiwa, kukatishwa tamaa na kuishi maisha yasiyo na uaminifu.

Kuenenda katika Roho inamaanisha kitu kingine kabisa. Inamaanisha kwa msaada wa Roho, tunajikumbusha kuwa Mungu alitubadilisha sisi. Tunaweza kuacha dhambi na kuchagua kufanya vitu sahihi badala ya

vitu vya kimwili vinavyotujia kwa asili. Mtume Paulo anasema "jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu" (Warumi 6:11). Tunahitaji msaada wa Roho kuishi kama wafu kwa dhambi. Paulo anasema "kwa Roho tunayafisha matendo ya mwili" (Warumi 8:13).

Uchaguzi wa kuenenda kwa Roho badala ya kuenenda katika mwili kunatuchangamotisha mara nyingi kwa siku. Mpaka Yesu anarudi, mwili wa mwanadamu utashindana na Roho. Tuwe makini na kuchagua kumtegemea Roho. Kumtegemea yeye kunatupa uiwezo wa kufanya jambo sahihi badala ya kuingia kwenye dhambi.

**Muhtasari:**

Ingawa Mungu aliukunja ulimwengu kutokana na dhambi, hatuachi sisi peke yetu kwenye ulimwengu huu uliokunjwa. Mungu alimtuma mwana wake, Yesu, kutuokoa kutoka kwenye dhambi na kutukomboa kutoka kwenye ulimwengu wa giza. Tunapopokea ukombozi huu kwa Imani, Roho Mtakatifu anakuja na kuishi ndani yetu. Anatusaidia kugeuza mioyo yetu kwa kutuwezesha kuishindana na mwili.

## Maswali: Sura ya Tano

1. Tumejifunza kuwa tunaweza kuishi kwenye ulimwengu uliokunjwa kwa kumtegemea Roho Mtakatifu kuusaidia kufanya chaguzi nzuri. Ni chaguzi gani unakutanza nazo kila siku? Kwa mfano, huwa unawatendea watu wengine vibaya unaposhindwa kupata njia yako mwenyewe?

2. Huwa unamuimba Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu akusaidie kufanya uchaguzi mzuri hata wakati unapokua hujisikii kufanya kitusahihi?

   Andika sentensi moja ya maombi hapa.

3. Orodhesha baadhi ya mifano ya jinsi unayosahau kumtegemea Roho Mtakatifu kwenye maisha yako.

# SURA YA SITA

## Ufalme wa Mungu Katika Udhihirisho

Mtazamo wa kibiblia kuhusu ulimwengu unatusaidia kufahamu ulimwengu wetu na kutufundisha nmna ya kuishi kibiblia ndani yake. Tunajua Mungu aliumba ulimwengu ukiwa mzuri. Ijapokua aliukunja baada ya kuasi kwa Adamu na Hawa, bado anatamani kutubariki na kutusaidia kuishi maisha ya utauwa.

Hii inamaanisha nini kwenye maisha ya kila siku? Kuwa mkristo na kuwa na mtazamo wa kibiblia juu ya ulimwengu inamaanisha kuacha maadili ya ulimwengu huu wa giza. Inamaanisha kujifunza maadili ya Mungu na kufuata namna mpya ya kuwa mwanadamu, ambayo Yesu Kristo alitutolea mfano. Inatupasa kumuiga Kristo kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

Kukomaa kama mkristo hakutokei papo kwa hapo. Fikiria mwembe, maembe yanaiva baada ya muda fulani. Yanakomaa na kukua kupitia

virutbisho vinavyotolewa kupita mti. Kukua kwa mkristo kunaweza kufananishwa hivyo.

Mkristo huendelea kuiva na kukomaa wakati wote. Ingawa hatufikii ukomavu kamili hapa duniani, tunapaswa kuendelea kupambana kukua katika mahusiano yetu na Mungu. Tunafanyaje hivi? Tunatakiwa kujirutubisha wenyewe kwa kusoma Biblia na maombi. Biblia inatufundisha jinsi Yesu alivyoishi na pia inatufanya kuelewa namna ya kuomba kibiblia.

Basi tufikiri kuhusu maombi kidogo. Utamaduni mmoja unaweza kuona maombi kama njia ya kumdhibiti au kumuendesha mungu[3]. Hata hivyo, Ukristo unamuona Mungu wa kweli kama Bwana ambaye kwake tunasujudu na kuwasilisha maombi yetu. Tusisahau kuwa yeye anatawala kama Mfalme wa ulimwengu wote.

Kumbuka nilisema kuwa hatufikii ukomavu kamili hapa duniani. Habari njema ni kuwa tunaweza kumtumikia Mungu huku tukiwa tunakua. Si kama embe ambalo ni lazima liive kabla ya kufurahiwa, hatuhitaji kufikia ukomavu kamili kabla Mungu kututumia. Tunaweza kuishi kwa ajili yake na kumtumikia tangu siku ya wokovu hadi siku ya kwenda nyumbani, mbinguni.

**Vipi Kuhusu Utamaduni?**

Mwanzoni mwa kitabu hiki nilizungumza kuhusu utamaduni na namna gani utamaduni tunaokulia unavyoweza kutengeneza namna tunavyojifikiria na kufikiria ulimwengu unaotuzunguka. Hii ni kwamba, utamaduni unaunda namna yetu ya kuutazama ulimwengu. Tunapomwamini Yesu lazima tutathmini na kufahamu utamaduni wetu. Hii inatusaidia kuchunguza maeneo ya mtazamo wetu wa ulimwengu yanayoendana na yasiyoendana na mtazamo wa kibiblia.

Watu wanoishi gizani wanawezaje kuona maana ya injili na mgeuko wa maisha? Jinsi waaminio wanavyoishi wakionyesha namna wanayomuiga Yesu, wanafanya ufalme wa Mungu kuwa wazi. Jinsi tunavyoishi inawapa wengine picha ya tabia ya Mungu.

Kukua kama mkristo na kumfunua Mungu kunaleta mapambano. Hata hivyo tunakutana na vishawishi kila siku. Vishawishi vinapokuja tunahitaji kujua kuwa mwili unatutaka tufanye kinachokuja kwa asili kufanya dhambi. Tunapotambua hili, Roho Mtakatifu anaweza kutusaidia kuishinda dhambi na kuchagua kumuiga Yesu.

Kama mfano, kuonesha ukarimu pale tunapokua hatujajua nia yetu inafanya tabia ya Mungu kujidhihirisha. Kwa upande mwingine, kumdhalilisha mtu kwa hasira kunafanya tabia ya mwili idhihirike. Kuathiri utamaduni kwa ajili ya Kristo, tunatakiwa kuhakikisha tunaendelea kumruhusu Mungu kugeuza mioyo yetu, itakayopelekea matendo ya utauwa.

**Kutoka Gizani Kwenda Nuruni**

Wokovu una maana zaidi ya kupandikiza imani mpya juu ya Imani ya zamani. Una maana zaidi ya kuongeza tabia na mila mpya kwenye maisha yetu mfano ubatizo, komunio au kuhudhuria kanisani. Kuwa mkristo inamaanisha kugeuka kutoka njia moja ya maisha na kugeuka kuelekea njia nyingine ya maisha. Wokovu unamaanishaa kuacha mfumo wa Adamu wa zamani (dhambi) na kufuata mfumo wa Adamu mpya, Yesu Kristo. Paulo anatwambia hili katika Waefeso:

> Basi nasema neno hili na nashuhudia katika Bwana, kwamba msiishi tena kama mataifa waishivyo-wenye akili za ubatili na ufahamu uliotiwa giza, wametengwa na uzima wa Mungu. Ujinga wao unatoka

> kwenye usugu na ugumu wa mioyo yao. Wamejitia katiak kutojizuia ili wafanye kila aina ya uchafu kwa tamaa.
>
> Lakini hamkujifunza hivi kwa Kristo (kama kweli mlisikia na kufundishwa kweli kuhusu Yesu)-ya kwamba weka mbali mwenendo wenu wa kwanza, utu wa zamani unaoharibika kwa tamaa zidanganyazo na mfanywe upya katika roho ya nia zenu na mvae utu mpya ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatiful uletwao na kweli. (Waefeso 4:17-24)

Kama ambavyo tumeshaona, Biblia inaonesha watu wasio amini kama raia wa ufalme wa giza (Wakolosai 1:13; Matendo 26:18). Hawajui chochote Zaidi ya giza. Giza kwao linaonekana ni kawaida. Watu wanaoishi kwa namna hii wamefarakana na Mungu kwenye maisha yao. Hii inawaacha wakiwa na nia batili na ufahamu uliotiwa giza na ujinga kuhusu kweli muhimu.

> …Hawamtukuzi Mungu wala hawamshukuru, lakini wamekua batili

> kwenye mawazo yao na mioyo yao yenye ujinga imetiwa giza...kwa hiyo Mungu akawaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu hata wakavunjiana heshima miili yaomiili yao. (Warumi 1:21, 24)

Nini kinapenya katika hili giza? Nuru ya injili pekee ndio inaweza kupenya na kuruhusu watu kufahamu kiuhalisia.

> …Mungu aliyesema "Nuru na ing'ae kutoka gizani" ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu kwa nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wake Kristo. (2 Wakorintho 4:6)

> Alituokoa kutoka kwenye utawala wa giza na kutuingiza katika ufalme wa mwana wake mpendwa. (Wakolosai 1:13)

Mungu alisema iwe nuru ikawa wakati wa uumbaji. Na baada ya hapo, Mungu huangazia nuru ndani ya mioyo ya watu wengi ambao hapo mwanzo hawakuujua ufalme wake. Watu waliotembea katika giza sasa wmesimama

katika nuru. Watu waliomtii mungu wa ulimwengu huu sasa wanamtii Yesu Kristo

Watu wanapomwamini Yesu, tunatumaini kuwa hatuweki Injili juu ya mtazamo wa kiulimwengu uliokuwepo, bali tunatumaini Injili inaondoa kabisa mtazamo wa ulimwengu usio sahihi na kuweka msingi mpya.

**Namna ya Kuishi Nuruni**

Roho Mtakatifu anatupa nguvu kubadilisha ndani kwenda nje na kutusaidia kuishi kwenye nuru. Mtu anayeenenda kwa Roho hukataa kuficha kilicho ndani yake.

Mtu huyu hajitahidi kwa nguvu zake kutaka aonekane ni mtu bora kwa nje tu. Mungu anataka mioyo yetu an matendo yetu yageuzwe. Yeye hataki sisi tuwaze na kuishi kama kila mmoja anayetuzunguka. Tunapojua yote Mungu aliofanya kwa ajili yetu, je hatupaswi kutaka kujitoa wenyewe kwake kwa unyenyekevu ili abadilishe matendo yetu yafanane na mtazamo wa ulimwengu wake?

Paulo anatusaidia kufahamu nini maana ya kumruhusu Roho Mtakatifu kutusaidia kukua. Kwa kweli anazungumza moja kwa moja na kwa nguvu kuhusu uhitaji wetu wa kuabdilika na kuishi maisha ya utauwa.

> Basi, ndugu zangu nawasihi kwa kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu. Ya kumpendeza Mungu ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe nbamna ya dunia hii bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu mpate kujua hakika mapenzi ya Munguyaliyo mema, ya kupendeza na makamiilifu. (Warumi 12:1-2)

Biblia inatangaza mawazo ya Mungu na kutusaidia kuona maisha kutokea kwenye mtazamo wa Mungu. Kwa sababu hii, tunahitaji kusoma Biblia mara kwa mara na kuitafakari kwa kina. Waaminio wanatakiwa kutafuta kujifunza kutoka kwa wale wanaoifahamu Biblia vizuri. Baada ya muda, hii huwa inabadili namna ya kuutazama ulimwengu.

**Mfano Uliopo wa Badiliko hai Kwenye Ndoa**
Injili haiangazii tu njia ya kuuelekea msamaha na uzima wa milele. Inafunua njia mpya na bora ya kuishi na kuruhusu wengine wamuone Mungu. Waaminio kwa msaada wa Roho Mtakatifu, wanatakiwa kumuonesha Mungu

kwa jinsi wanavyochagua kuishi. Huu ni wajibu mkubwa. Tafakari mazingira haya.

Ingekuaje kama kwenye ndoa:

- Wakristo wangejulikana kama raia bora kwenye kijiji, mji au nchi- sio kwa sababu ya maneno yao bali kwa sababu ya matendo yao?
- Wanaume wakristo wangejulikana kama viongozi watumishi wanaopenda wake zao kwa kujidhabihu, ambao kwa kawaida wanaweka chini matamanio na matakwa yao ili kutimiza mahitaji ya wake zao?
- Wanawake wakristo wangewapenda waume zao kwa shauku wakitafuta kuwajenga na kuwatendea kwa heshima?
- Wakristo wote wangeishi kwa dhati kama watu wa Mungu kibinafsi, nyumbani na kwenye jamii ya kikristo?

Wakati mwingine mtazamo wa ulimwengu kibiblia na mtazamo wa ulimwengu kiutamaduni vinagongana. Hii ni kweli katika ndoa na katika maeneo mengi ya maisha yetu. Mgongano unapotokea, tuna uchaguzi. Je tunachagua kumfunua Mungu kwa kutenda kwa namna ambayo anasema ni sahihi au

tunachagua kufuata utamaduni wetu? Hebu tangalie mifano miwili:

- Utamaduni unaposema, “mke yupo ili kutimiza tamaa ya ngono kwa mume wake” mwanamume mkristo anajua namna ya kuomba kwa upendo kushiriki tendo la ndoa na mke wake badala ya kutumia nguvu.
- Utamaduni unapposema, “mwanamume mkubwa ni yule mwenye watoto wengi (au ana wanawake wengi)” mwanamume mkristoanafuata mfumo wa mwanamke mmoja ulioanzishwa na uumbaji wa Adam na Hawa.

**Israeli na Sisi-Jamii Zilizogeuzwa**

Kwenye agano la kale, Mungu alikusudia taifa la Israeli liwe kama sumaku. Kama taifa lingeishi tofauti na mataifa mengine yanayolizunguka, basi wangevuta umakini wa mataifa mengine. Wageni wangekuja kuangalia kwa ukaribu hili kundi la ajabu la watu lisilofanana na mengine. Musa aliwaambia Israeli:

> Angalieni, nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama Bwana, Mungu

> wangu alivyoniamuru ili mzitende katika nchi mwingiayo ili kumiliki. Nawe ukazitende kwa bidii, maana hii ndiyo hekima na akili zenu mbele za watu. Watakapozisikia hizi amri, watasema, "Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili." (Kumbukumbu 4:5-6)

Tatizo? Nyakati nyingi Israedli walishindwa kuwa tofauti. Waliishi vibaya kama wengine na wakati mwingine vibaya Zaidi kuliko wao. Kwa kweli, nabii Isaya alisema kwamba kwa sababu ya jinsi ulivyoishi Israel "mchana kutwa, Jina la Mungu limetukanwa!" (Isaya 52:5).

Kwenye Agano Jipya, Mungu anamtuma Roho Mtakatifu kuishi ndani ya watu wake. Kama tukitii uongozi wake kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, mioyo yetu yaweza kupokea badiliko. Sasa ni wakati wetu kubadilisha jamii. Kama waaminio tukichagua kuishi utauwa, nuru ya Mungu itaangaza nje kwa watu wapate kuiona. Kwa namna hii, aidha kwa ndoa zetu au maeneo mengine ya maisha yetu, tunamdhihirisha Mungu na kuleta Injili-Nuru ya kweli kwenye huu ulimwengu uliotiwa giza.

**Muhtasari**

Tukumbuke kuwa Mungu anajari uumbaji wake. Anatutaka tuwe na mahusiano ya karibu naye. Kama waaminio, ametupa pasipoti mpya na makao mapya. Amemshinda adui yetu, shetani, na ametupa Roho Mtakatifu kubadilisha kuwaza na kutenda kwetu.

Tunatakiwa kufanya nini na hizi habari? Tunatakiwa tumshukuru Mungu mwenye nguvu kwa kutupenda. Tunatakiwa pia kumuiga Yesu ili tuive au tukomae kama embe lenye ladha nzuri. Tusikilize uongozi wa Roho Mtakatifu ndani yetu tunaposoma Biblia na kuomba. Ishi maisha yanayooneha mtazamo wa ulimengu kibiblia na kuruhusu Imani potofu za kitamaduni kuondoka na tuwafundishe wengine.

## Maswali: Sura ya Sita

1. Kama wakristo lazima tujifunze kumuiga Yesu. Unafikiri watu wengine wanamuonaje Yesu wanapoyatazama maisha yako?

2. Utamaduni wako unapokufundisha kuufanya kitu fulani lakini Neno la Mungu likawa linakwambia ufanye kitu kingine, utachagua kipi? Kumbuka kuwa Mungu huwapa waaminio Roho wake Mtakatifu kuwasaidia kufanya uchaguzi sahihi wanapokutana na mazingira haya.

3. Orodhesha mfano mmoja ambapo utamaduni wako unaweza kugongana na kweli ya Neno la Mungu. Omba sasa kwamba utakumbuka kuomba nguvu ya Mungu ikusaidie kufanya uchaguzi sahihi.

# HITIMISHO

Wote tunakua tukiwa na mtazamo wa ulimwengu. Swali ambalo kitabu hiki linaibua ni kwa namna gani tunaweza mtazamo wetu wa ulimwengu unaweza kubadilika tunapomwamini Yesu? Je tunapandikiza elimu mpya ya Mungu juu ya vitu ambavyo tulikua tunaviamini tayari au tunajitathimini upya ni nin utamaduni wetu umetufundisha na kutupilia mbali mawazo yasiyo sahihi?

Kumbuja kuwa kila utamaduni unatazama ulimwengu kwa usahihi na kwa isivyo sahihi pia. Tunatakiwa kukubaliana na maadili ya kweli na kukabiliana na maadili yasiyo sahihi, hata kama italeta mwitikio hasi kutoka kwa wengine. Kwa namna hii tunamheshimu na kumdhihirisha Mungu kwenye familia zetu, makanisa na jamii.

Tumeona kwamba kuishi sawsawa na mtazamo wa kibiblia unaweza kuleta changamoto. Tunahitaji kuweka kweli hizi karibu na mioyo yetu:

- Tuna adui anaitwa shetani. Bado Mungu anatawala juu ya hiki kiumbe hata kama anajaribu kusambaza uongo wake na kuwaweka watu katika vifungo. Kwenye ulimwengu huu wa giza tunahitaji kusimama imara kinyume na uongo wa shetani.
- Ulimwengu unabaki umekunjwa, au giza kwa sababu ya dhambi. Mungu siku moja atanyoosha na kurejesha upya uumbaji wake. Lakini mapak wakati huo tunahitaji kuishi maisha ya utauwa kwenye ulimwengu uliotiwa giza.
- Roho aliyetolewa kwa waaminio wote, anatsaidia kuishi njia ya Mungu na kusema hapa kwa dhambi ndani yetu wenyewe. Ili hilo litokee tunahitaji kumruhusu Mungu atufundishe na kutuongoza.
- Kukomaa kwa mwamini katika Yesu kunatokea tunaposoma Biblia kwa uaminifu na kuomba.

Tukifuata amri ya Mungu kueneza Injili na kuwafundisha wengime, kubadilisha mtazamo wetu wa ulimwengu upate kufana na matazamo wa Mungu, hilo ni muhimu.

Kumbuka mganga wa kienyeji na wateja wake mwanzoni mwa hiki kitabu. Ingekuaje kama kila mtu aliyeomba maombi ya Imani siku ile angekua katika ufahamu wa kweli za Mungu na kutupilia mbali Imani potofu? Wote wangemdhihirisha Mungu hata kama ingewagharimu kazi au vitu vingine. Fikiria jinsi ambavyo mabadiliko ndani ya hawa waaminio yangeathiri kila mmoja aliyewazunguka, labda kuwatoa wengi kwenye vifungo na kuwaingiza kwenye uhuru wa Imani katika Mungu.

Vipi kuhusu wewe? Utamwamini Mungu kuhusu kesho yako? Utatupilia mbali Imani zako potofu hata kwa gharama? Uko tayari kuishi sawasawa na mtazamo wa kibiblia na kueneza kweli ya Mungu? Kama ndivyo, basi tuendelee kueneza habari njema na kumdhihirisha Mungu kwa maisha yetu.

# Habari Njema kwa Ajili Yako

Kitabu hiki kimeonesha baadhi ya hali halisi za kikatili za maisha ya humu ulimwenguni. Pia kinaonesha Mwana wa Mungu, Yesu Kristo kama tumaini letu la kuishi maisha ya utauwa badala ya magumu tunayokutana nayo ulimwenguni.

Kitabu kinaongelea kukua katika mahusiano na Yesu. Namna gani tuaweza kufanya hivi? Tunawezaje kujua kwa hakika kuwa kwamba dhambi zetu zimesamehewa na tutaishi na Yesu milele maisha yetu hapa duniani yakiisha?

Biblia inatuambia "Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka-wewe na nyumba yako" (Mdo 16:31). Hii inamaanisha nini hasa? Hebu tupitie maandiko mengine ili kuuelewa mstari huu vizuri Zaidi.

- Biblia inatufundisha kuwa hapo mwanzo Mungu aliumba ulimengu kamili na akasema kuwa ni vyema sana (Mw 1:1, 31).
- Wanadamu ambao Mungu aliwaumba na kuwaweza kwenye ulimwengu walimuasi. Na wakati huo huo dhambi ikaingia

ulimwenguni na ikatutenga mbali na Mungu (Mw 2:4-3:24).

- Bado Mungu anataka mahusiano na uumbaji wake na anatupenda kila mmoja wetu. “Kwa jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila kila amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele” (Yn 3:16).
- Kuja kwa Mungu, kwanza tunahitaji kutambua kuwa tunaishi mbali na yeye. “Kwa maana wote tumetenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu” (Rum 3:23).
- Hii hapani habari njema ya Injili: Mungu alimtuma Mwanawe, Yesu kufa msalabani na kulipa gharama ya dhambi zetu. Alizikwa na akafufuka kutoak katikawafu siku ya tatu, akashinda mauti na dhambi. “Lakini Mungu anadhihirisha upendo wake kwetu katika hili: tungali wenye dhambi, Kristo (Yesu) alikufa kwa ajili yetu” (Rum 5:8).
- Tunaweza kukubali malipo ya dhambi zetu aliyoyafanya Yesu kwa ajili yetu. Tunaweza kumwamnini kutuokoa kutoka kwenye dhambi zetu na kutuingiza kwenye mahusiano na Mungu. “Kwa maana

mmeokolewa kwa neema kwa njia ya Imani ambayo hikutokana na nafsi zenu bali ni kipawa cha Mungu-si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Efe 2:8-9).

**Namna ya Kupokea Kipawa cha Wokovu**

Hitaji pekee la kupokea kipawa hiki ni kuamini hizi kweli:

1) Mungu alituumba na anatupenda.
2) Kila mmoja wetu amezaliwa na dhambi na tunaendlea kutenda dhambi maisha yetu yote.
3) Yesu alikufa na alilipa gharama kwa ajili ya dhambi zetu.
4) Yesu kwa kifo na ufufuko wake ametupa zawadi ya msamaha.
5) Tunapotubu (kugeuka kutoka kwenye dhambi) na kukubali wokovu (kugeuka kumuelekea Mungu kutuokoa) tunakua sehemu ya familia ya Mungu milele.

**Mfano wa Maombi Kwa Ajili ya Wokovu**

Mungu nakushukuru kwa kunipenda na kumtuma Mwana wako afe msalabani kwa ajili yangu. Ninatambua mimi ni mwenye dhambi na ninahitaji msamaha wa dhambi zangu. Ninakubali malipo ya Mwana wako kwa ajili

ya dhambi zangu pale msalabani. Ahsante kwamba Yesu ulishinda mauti na ukafufuka kutoka kwa wafu. Ahsante kwa kunikubali katika ffamilia yako na kuisha pamoja na wewe milele. Naomba unisaidie kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu ninapoishi hapa duniani.

# MWISHO

1 Edwin M. Yamauchi, “Magic in the Biblical World,” *Tyndale Bulletin* 34 (1983), 174-75.
2 Paul G. Hiebert, *Transforming Worldviews: An Anthropological Understanding of How People Change* (Grand Rapids: Baker, 2008), Kindle locations 542-544.
3 Hiebert, Kindle Locations 6348-6349